# NYWILA

*******

**ILI NDOA ISIKUSHTUE**
**TAMBUA HAYA!**



JAMES KALEKWA

# NYWILA:

*Ili ndoa isikushitukize, tambua yafuatayo.*

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

Nywila #1: MSINGI WA NDOA ........................................ 4

NDOA KAMA UJENZI WA NYUMBA: ........................................ 5

Nywila #2: KUACHA, KUSAHAU NA KUAMBATANA. ............. 10

Kuacha siyo nini? ........................................ 11

Nywila #3: TASWIRA YA KRISTO NA KANISA ........................ 17

Mke: ........................................ 18

Mume: ........................................ 19

Mkazo muhimu: ........................................ 19

Kuhusu Mwandishi: ........................................ 20

Kuhusu New Vine Church: ........................................ 21

Mawasiliano na Mwandishi: ........................................ 21

# Nywila #1: MSINGI WA NDOA

*"Kama misingi ikiharibika, Mwenye haki atafanya nini?"*
**Zaburi 11:3**

*Msingi ndiyo huamua uimara wa jengo.*
*Msingi ndiyo huamua muundo wa jengo.*
*Msingi ndiyo huamua aina ya jengo.*
*Msingi ndiyo huamua ukubwa wa jengo.*

Msingi ndiyo kila kitu.

Ukiuona msingi, unaweza ukatabiri kuhusiana na jengo. Kwa hiyo, aina ya jengo huamua aina gani ya msingi uwepo. Mnara huamua uwepo msingi wa mnara; ghorofa huamua tuanze na msingi wa ghorofa; na kibanda hutusukuma tuanze na msingi wa kibanda.

Ndivyo ilivyo kweli kwenye ndoa.

Kama misingi ikiharibika, mwenye haki hana la kufanya.

Basi, kabla ya kushughulika na chochote kwenye jengo la ndoa. Hebu turudi kutazama msingi.

## NDOA KAMA UJENZI WA NYUMBA:

Biblia imefananisha ndoa na ujenzi wa nyumba.
*"Nyumba hujengwa kwa hekima, Na kwa ufahamu huthibitika,"*
Mithali 24:3

Tena, imefananisha maisha kwa ujumla wake (ndoa ikiwemo) na ujenzi wa nyumba
*"Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba;"*
Mathayo 7:24

Kwa kuanzia kabisa, tunakubaliana na kweli ya neno la Mungu ya kwamba ndoa si bahati au haiibuki tu kama uyoga... INAJENGWA!

Hakuna ndoa inayoibuka kama zali la mentali... HAKUNA! Hakuna zali kwenye ndoa. Kila kitu ni matokeo ya kujua na kukusudia.

Pili, tunakubaliana ya kwamba NDOA inajengwa kwa MAARIFA na inathibitishwa kwa UFAHAMU... Hivyo ndiyo vifaa vya kujengea ndoa.

Kama watu wasemavyo, mwili haujengwi kwa sementi na matofali; kadhalika ndoa... hujengwa kwa MAARIFA na kutihibitishwa na UFAHAMU.

Na kwa mujibu wa neno la Mungu (Mathayo 7:24), BUSARA/HEKIMA ni KUSIKIA NENO LA MUNGU na KULIFANYA... kwanza, unasikia; pili, UNATENDEA KAZI.

Ndiyo ndoa inajengwa hivyo!

### Msingi #1. NDOA NI WAZO LA MUNGU.

Ni kweli kuna tamaduni na mapokeo kuhusiana na ndoa; kuna falsafa, elimu na mitazamo mbalimbali kuhusiana na ndoa.

Ukweli ni huu, ndoa ni wazo la MUNGU. Alilibuni na kuiasisi Yeye mwenyewe.
*"Bwana Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye."*
**Mwanzo 2:18**

Hakuna ndoa ya taifa au utamaduni fulani.

Hakuna ndoa ya kabila fulani.

Hakuna ndoa ya kada fulani ya watu.

Ndoa ni ya Mungu.

Yaani, hakuna ndoa za kizungu na kienyeji, kimila, kiafrika ... hakuna ndoa za kabila letu (weka jina la kabila lako hapo); hakuna ndoa za wenye elimu na

wasio na elimu; hakuna ndoa za watu wa daraja fulani.

Ndoa ni wazo la Mungu... BASIII!!!

Umeshawahi kusikia wanandoa wanasema "Ndoa zetu sisi wasukuma huwa ziko hivi na vile..." (nimeandika kabila ninalotokea ili mtu asione ninashambulia kabila yake). AU "... sisi watu wa mkoa wa Mara huwa hatuna ndoa za namna hiyo" (nimetumia kabila la mke wangu ili nisishambulie makabila ya wengine.)

Tena utasikia wanandoa wanataka kuwa na ndoa *"ya kizungu..."* au *"ndoa ya kisomi"*

Ndoa ni wazo la Mungu.

Ili ndoa ijengeke vyema ni lazima ijikite mizizi kwenye hiyo kweli.

### Msingi #2 WAZO LA MUNGU; NJIA YA MUNGU.

Ili tuone na kufurahia matokeo ya ndoa ni vizuri tufahamu ya kwamba wazo la Mungu litatekelezwa kwa njia ya Mungu.

Kwa ujumla, wengi tunaweza kukubali ndoa ni wazo la Mungu lakini tusikubaliane na njia yake ya ujenzi wa ndoa... tukataka kutumia njia zetu.

Nikisema kwa mifano; unakubali kuwa na ndoa lakini unataka auijenge "kisukuma AU kikurya" au (weka jina la kabila lako zuri hapo).

Kama tumekubali ya kwamba ndoa ni wazo la Mungu, basi tulifuate mpaka mwisho (follow through) ili tufurahie matokeo ya ndoa zetu.

Kwa uelewa huo ni kwamba, ninapaswa kuweka mbali mitazamo yoyote, elimu, falsafa, mila na desturi na kubaki kwenye ukweli mmoja... NDOA NI WAZO LA MUNGU!

## Msingi #3: MAMBO KADHAA YA KUFAHAMU KUHUSU NDOA WAZO LA MUNGU.

1. Ndoa ya mwenzi mmoja (Mwanzo 2:18) - Mungu alimfanyia Adamu msaidizi na siyo wasaidizi. Ndoa yenye mguso chanya ni ile ya mwenzi mmoja (pande zote mbili). Mwenzi mmoja hadharani, na sirini!

2. Ndoa ya wenzi sawa (equal partners) - ni vizuri kujua ya kwamba wenzi wanaoingia kwenye ndoa ni sawa (equals). Mwanzo 1:26-28... ndoa si baina ya baba na binti AU mama na kijana; au mwenzi mmoja anamuona mkubwa kuliko mwenzake... HAPANA! Vilevile ndoa si huruma au hisani ...

huyo mwanamume au huyo mwanamke kuolewa na wewe si kama umempa msaada. Ninyi ni EQUALS!

3. Ndoa ina muundo wa kimamlaka na majukumu (hierarchical) ... si ukumbi wa hovyo na usiokuwa na mpangilio. [Rejea: Waefeso 5:21-33]

    a) Wenza sawa [Rejea: Waefeso 5:21]
    b) Nafasi na majukumu ya mke [Rejea: Waefeso 5:22-24]
    c) Nafasi na majukumu [Rejea: Waefeso 5:25-33]

4. Ndoa HAINA MWISHO Rejea Mathayo 19:8 - Tangu Mwanzo Mungu hakukusudia kuachana (talaka) isipokuwa ni ugumu wa mioyo ya watu. Tena kwa neno lake anasema anachukia kuachana (talaka); anawapenda wanadamu hata wanaoachana ila ANACHUKIA KUACHANA (Malaki 2:16)

# Nywila #2: KUACHA, KUSAHAU NA KUAMBATANA.

Ndoa ambayo ni WAZO la Mungu huwa na sifa ya "kuacha"

A. Mwanamume anapaswa kuwaacha baba na mama yake (wazazi wake).

*"Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja."*

**Mwanzo 2:24**

Kama mwanamume hawezi kuacha, hawezi kuwa mume; na mwanamke aliyeolewa na mume ambaye hajaacha huwa hakai kwa utulivu na ridhiko (anajiona hajafika bado).

**Kuacha ni nini?**

Kuacha ni kubadilisha mkazo na vipaumbele vya kimahusiano baina ya mwanamume na wazazi wake. Kimsingi, kila mwanadamu ni matokeo ya wazazi wawili kukutana kimwili na kulea. Inatarajiwa ya kwamba, mtu atalelewa na kuishi na wazazi/walezi wake mpaka umri fulani wa ukubwa/ukomavu. Hivyo, wazazi/walezi ni watu ambao anaishi nao muda mrefu kuliko mtu mwingine yoyote.

Ili ndoa iwe na matokeo, mwanamume anapaswa KUBADILI mkazo, kipaumbele nafasi ya kimahusiano

baina yake na wazazi wake.

Kabla ya NDOA, mwanamume huhusiana kwanza na Mungu, kisha wazazi kisha watu wengineo; LAKINI baada ya ndoa, mwanamume huhusiana na Mungu kwanza kisha mke wake halafu wazazi na wengineo wanafuata.
Umeona huo mpangilio/mtiririko?

Kama Mungu amesema unawaacha wazazi maana yake anajua unaweza na ametoa hiyo neema.

Na hapa naomba niweke sawa. Kuacha huku si kwa sababu ya ugomvi, chuki au maumivu... ni kutii NENO LA MUNGU tu! Nothing personal!

Hebu fikiria hivi, kama unaweza kuwaacha wazazi basi unaweza kumuacha mtu mwingine awaye yote. Unaweza kuwaacha ndugu, jamaa na marafiki... inaweza ukawaacha classmates, na colleagues wa kazini kwako... kama unaacha wazazi, basi wengine unapaswa kuwaacha bila kuuliza.

Kumbuka, tafsiri ya kuacha ni KUBADILISHA MKAZO, NAFASI NA VIPAUMBELE VYA KIMAHUSIANO.

## Kuacha siyo nini?

Kuacha si kuhama nyumbani na kuishi chumba/nyumba mpya ya kupanga; kuacha si kutojali wazazi; kuacha si kuwakosea heshima wazazi; kuacha si kuingia kwenye magomvi na wazazi.

### Jihadhari:

Usipoacha (hata kama ufanye kisirisiri) mke wako atajisikia kupwaya na kukosa nafasi yake stahiki. Anaweza asiwe na maelezo juu ya kujisikia kwake lakini ni kwa sababu kwenye hiyo ndoa hajapewa nafasi yake - HAJAOLEWA!
Bado uko na wazazi, ndugu, jamaa na marafiki n.k
Mahusiano ni swala la moyo. Ni zaidi ya viapo na vyeti vilivyosainiwa. Kama umeacha itajulikana. Kama unafanya usanii au umeacha kisanii itajulikana pia.

Matokeo ya kuacha yataonekana kwa mwenzi wako na kwa ndoa yenu.

### B. Mwanamke napaswa kuwasahau watu wa nyumba ya baba yake.

*"Sikia, binti, utazame, utege sikio lako, Uwasahau watu wako na nyumba ya baba yako.*
*Naye mfalme atautamani uzuri wako, Maana ndiye bwana wako, nawe umsujudie."* **Zaburi 45:10-11**

Ulishawahi kusikia mtu anasema samehe na usahau?

Huwa unaweza kusahau?

Maana ya kusahau kwenye dhana ya msamaha, ni kusamehe kiasi kwamba hata ikitokea mtu akakukumbusha au wewe ukakumbuka ulikosewa hauumii bali unakumbuka ya kwamba ulisamehe. Lakini tukio hulisahau. Lakini haliumi kwa sababu unakumbuka ulisamehe.

Ndivyo ilivyo kuwasahau watu wa nyumba ya baba yako.

Si kuwapotezea! Siyo kufuta mawasiliano! Si kutosalimiana nao!

Bali, kila ukiwakumbuka unafahamu ya kwamba umeolewa na mume wako ndiye wa kwanza kwenye moyo wako baada ya Mungu.

Ajabu na kweli ni hii, Biblia inasema ukiwasahau watu wa nyumba ya baba yako ndipo mfalme (mume wako) atautamani uzuri wako... Hii ni kweli nzito sana.

Yaani, unaweza ukapaka make up kirikuu nzima; unaweza ukapuliza perfume ya dollar elfu nyingi; unaweza ukazungusha kiuno kama feni na kujinyonga kitandani kama mnenguaji ... kama

hujawasahau watu wa nyumba ya baba yako, mumeo hatavutwa na uzuri wako.

Ili upendwe na umtamanishe mumeo, ni rahisi sana... WASAHAU WATU WA NYUMBA YA BABA YAKO.

Mwanaume anaweza kutaka sana kukupenda na kuvutiwa na wewe. Na anaweza akajitahidi kwa kujifunza, lakini moyoni inagoma tu. Huna uhalali wa moyo (legitimacy)... hana maelezo, anajikuta hawezi tu.

Kwa nini? Mahusiano ni swala la moyo. Ukiwasahau watu wa nyumba ya baba yako, atajua tu moyoni. Ataisikia nafasi yake stahiki iko wazi aichukue.

Umeshawahi kuona mwanamke mrembo dunia nzima lakini mume wake havutiwi naye? Moja ya sababu ni hii... bado moyo uko kwenye nyumba ya baba yake.

Kuwasahau watu wa nyumba ya baba yako ni KUBADILI vipaumbele na mikazo ya kimahusiano baina yako na nduguzo na kumpa mfalme/bwana wako nafasi yake stahiki.

Nalo hili ni swala la moyo.

### C. Baada ya kuacha na kusahau wenzi yanapaswa KUAMBATANA.

*"Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja."*
**Mwanzo 2:24**

Taswira ya kuambatana inayokujia kichwani ni ipi? Au ulipokuwa ukisoma Biblia au ukisikia mafundisho unatengeneza mental picture gani ya kuambatana?

Kutembea pamoja ufukweni, mmeshikana mikono, Mmevaa nguo za kufanana (twinning)... au mnatembea kwenda kanisani pamoja, mume amekubebea mkoba, na mwamvuli, na mmeshona nguo za vitenge zinazofanana...

Mnakuwa mnaambatana!!!

Ni kweli mnaambatana.

Lakini, Biblia haisemi hivyo.

*"Je! Watu wawili waweza kutembea pamoja, wasipokuwa wamepatana?"*
**Amosi 3:3**

Kumbe kutembea pamoja ni matokeo ya kupatana. Mioyo kukubaliana. Kunia pamoja, mamoja, kuongea lugha moja, kukubaliana misamiati.

Hiyo taswira uliyokuwa nayo kuhusu kuambatana ni kweli, lakini ni matokeo tu. Kwa hiyo, kuna kiini cha kuambatana.

Ili ndoa iwe na mguso chanya LAZIMA mkubaliane na muelewane. Kumbuka, mnatokeao backgrounds tofauti; mna haiba tofauti; mna malezi tofauti... kukubaliana si jambo la fumba-fumbua. Ni mchakato. Inawezekana kuna mambo ni kawaida kwa mujibu wa malezi, elimu au utamaduni uliotokea. Lakini yakawa si kawaida kwa mwenzi wako. Ni lazima mshughulike nayo kuyayeyusha (iron out).

Hii itajumuisha kuacha misimamo, mitazamo, uelewa ili kukumbatia vipya! Itajumuisha kujidhabihu na kujikana... na jambo hili ni la pande zote mbili (mume na mke)

Hamuwezi kuambatana iwapo hamkubaliani juu ya maswala fulani.

- ✓ Maswala ya IMANI na maisha ya kiroho.
- ✓ Vipi kuhusu ndoa na familia.
- ✓ Kuhusu malezi ya watoto.
- ✓ Kuhusu uchumi na fedha.
- ✓ Kuhusu ndugu, jamaa na marafiki
- ✓ Vipi kuhusu kushughulikia tofauti/migogoro baina yenu.

Unaona, ni kama mnaunda kijikatiba fulani cha kuongozea nchi yenu.

Tena hata kwenye mambo ambayo bado mko kwenye mchakato wa kuyashughulikia, mnakubaliana kutokukubalia na mnapendana huku mkiyashughulikia.

KUAMBATANA!

Umeshawahi kuona wenzi wameshona sare na ukiibua swala la fedha unaona wanageuka maadui. Uadui mkubwa kiasi cha kutosemeshana au kutishia kuachana, kutosalimiana au kutowasiliana.

Hao wameoana kingono, na kutalikiana kwenye hilo eneo (sexually married, financially divorced).

Unaona ukubwa wa swala hili la kuambatana?

## Nywila #3: TASWIRA YA KRISTO NA KANISA

*"Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo."*
**Waefeso 5:24**

*"Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake;"*

**Waefeso 5:25**

Ndoa imekusudiwa kuwa uakisi (reflection) wa Kristo Yesu na kanisa. Mahusiano baina ya Yesu na kanisa yanapaswa kuonekana kwenye utekelezaji wa siku kwa siku kwenye ndoa.

## Mke:

Kwenye ndoa, mke ameaminiwa na Mungu kuwa mfano wa kanisa. Utii anaouonyesha mke kwa mume wake unapaswa kuwa fundisho la kivitendo kwa mume; ni kwa namna gani mume [ambaye ni sehemu ya kanisa/mke wa Kristo] anapaswa kuwa mtiifu kwa Kristo. Kwa hiyo, mke anapaswa kujua ya kwamba huo utii si tendo la hisani kwa mumewe, bali ni darasa.

Nionyeshe mume mtiifu kwa Kristo, nami nitakuonyesha mke mtiifu kwa mumewe.

Ukiona mume asiyekunjika mbele ya mamlaka ya Kristo, ujue hajawahi kuona mke anayekunjika mbele ya mamlaka ya mume.

Kuwa mke ni kuaminiwa kukubwa sana na Kristo. Umeaniwa kumtengeneza Yesu kwa vitendo kanisa lake.

Mke, kama huwezi kuwa mtii kwa "faida ya mume wako"; basi uwe mtii kwa faida ya kanisa na ufalme wa Mungu.

### Mume:

Ni jukumu la heshima sana umepewa kuwa mume. Umeaminiwa ufananishwe na Kristo mwenyewe. Mahala pekee kwenye ulimwengu wa mwili ambapo mkeo atajifunza ni kwa jinsi gani Yesu Kristo analipenda kanisa, ni kwako! Yaani, mkeo anapaswa kusikia upendo wa Kristo kwa kanisa [ambalo mkeo ni sehemu yake] kupitia wewe.

Binafsi, kila nikitafakari hivyo, huwa ninachukua swala la kuwa mume kwa hofu na machozi.

Nionyeshe mke anayefurahia pendo la Kristo, nami nitakuonyesha mume mwenye upendo kwa mkewe.

Ukiona mke anapata shida kuelewa na kufurahia pendo la Kristo, ujue hajawahi kuona udhihirisho wa pendo kutoka kwa mumewe.

### Mkazo muhimu:

Swala la utii kwa mume na upendo kwa mke si swala la kihisia. Ni kweli wanadamu tuna hisia. Lakini hisia huja na kuondoka; hupanda na kushukua. Hili ni swala la maamuzi ya kutii neno. Iwe unajisikia au haujisikii, unapaswa kutii na kutenda neno.

Ninakupa angalizo ya kwamba usitekeleze neno hili kwa kujisikia au kutokujisikia.

Na kila kutii maagizo ya Mungu huwa na thawabu inayoambatana na ahadi ya neno hilo.

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi n audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764


